ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1. Mhe. Ali Abdalla Ali	Naibu Spika/Jimbo la Mfenesini.
2. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Mwenyekiti wa Baraza Jimbo la Kikwajuni.
3. Mhe. Mgeni Hassan Juma	Mwenyekiti wa Baraza/ Nafasi za Wanawake.
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamu wa Pili wa Rais/Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Kuteuliwa na Rais.
5. Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora/ Jimbo la Dimani.
6. Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Fedha/ Kuteuliwa na Rais.
7. Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/Jimbo la Tumbatu.
8. Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa na Rais.
9. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais/ Kuteuliwa na Rais.
10.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
11. Mhe. Rashid Seif Suleiman	MBM/ Waziri wa Afya/ /Jimbo la Ziwani.
12.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Maakazi, Maji na Nishati/ Kuteuliwa na Rais.
13.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Kuteuliwa na Rais.
14.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa na Rais.
15.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni.
16.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge.
17.Mhe Dr. Sira Ubwa Mamboya	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Kuteuliwa na Rais.
18.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara,Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni.
19.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni Utalii na Michezo/Jimbo la Gando.
20.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma/Jimbo la Makunduchi.
21.Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni.
22.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.

23. Mhe. Shawana Bukheit Hassan	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Dole.
24. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka.
25. Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake.
26.Mhe.Mahmoud Thabit Kombo	Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki
27.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake.
28.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/ Jimbo la Nungwi.
29.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni.
30.Mhe. Mohammed Said Mohammed	Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Mpendae.
31.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake.
32.Mhe. Said Hassan Said	Mwanasheria Mkuu.
33.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
34.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
35.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
36.Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa na Rais
37.Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
38.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
40.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
42.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
43.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
44.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
45.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
46.Mhe. Hamad Masoud Hamad	Jimbo la Ole
47.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
48.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
49.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
50.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu	Jimbo la Bububu
51.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
52.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni

53.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
54.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
55.Mhe. Marina Joel Thomas	Kuteuliwa na Rais
56.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando)	Jimbo la Mkwajuni
57.Mhe. Mlinde Mabrouk Juma	Jimbo la Bumbwini
58.Mhe. Mohammed Haji Khalid	Jimbo la Mtambile
59.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali	Jimbo la Uzini
60.Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi	Jimbo la Chambani
61.Mhe. Mussa Ali Hassan	Jimbo la Koani
62.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Nafasi za Wanawake
63.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake
64.Mhe. Nassor Salim Ali	Jimbo la Rahaleo
65.Mhe. Omar Ali Shehe	Jimbo la Chake-Chake
66.Mhe. Panya Ali Abdalla	Nafasi za Wanawake
67.Mhe. Rufai Said Rufai	Jimbo la Tumbe
68.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake
69.Mhe. Saleh Nassor Juma	Jimbo la Wawi
70.Mhe. Salim Abdalla Hamad	Jimbo la Mtambwe
71.Mhe. Salma Mohammed Ali	Nafasi za Wanawake
72.Mhe. Salma Mussa Bilali	Nafasi za Wanawake
73.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni
74.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	Nafasi za Wanawake
75.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	Jimbo la Mwanakwerekwe
76.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni
77.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde
78.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	Jimbo la Jang'ombe
79.Mhe. Ussi Jecha Simai	Jimbo la Chaani
80.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
81.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake

Ndugu Yahya Khamis Hamad **Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

BARAZA LA NANE LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI NA NANE

Kikao cha Kwanza - Tarehe 21 Januari, 2015

(Kikao kilianza saa 3.00 Asubuhi)

DUA

Mhe. Spika,(Pandu Ameir Kificho) alisoma Dua

TAARIFA YA SPIKA

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe kwanza nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuwa hai, na leo tukamudu kufika katika shughuli zetu za Mkutano wa Kumi na Nane wa Baraza la Wawakilishi ambao unaendelea kuanzia leo tarehe 21/01/2015.

Taarifa ya Spika ya leo Waheshimiwa Wajumbe inahusu kazi ambayo mulizifanya huko nyuma, na kwa mujibu wa taratibu za Kanuni tunawajibika kuwapa taarifa kuhusu kazi yenu hiyo muliyoifanya.

Waheshimiwa Wajumbe katika Mkutano wa Kumi na Saba wa Baraza la Nane la Wawakilishi, uliofanyika kuanzia mwaka tarehe 22 hadi 31 Oktoba, 2014. Baraza lilipitisha Miswada minne ya Sheria kama ifuatavyo.

Mswada wa Sheria wa kufuta Sheria ya Wauguzi na Wakunga, uanzishwaji wa Baraza la Usajili la wauguzi na wakunga Na. 9 ya mwaka 1986, na kuanzisha badala yake Sheria mpya ya Wauguzi na Wakunga na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Mswada wa pili Waheshimiwa Wajumbe, ulikuwa ni Mswada wa Sheria wa kuanzisha Shirika la Nyumba la Zanzibar na mambo mengine yanayohusiana na hayo ya mwaka 2014.

Mswada wa tatu ulikuwa ni Mswada wa Sheria ya kufuta Sheria ya Baraza la Manispaa Na. 3 ya mwaka 1995 na Sheria ya Halmashauri ya Wilaya na Mabaraza ya Miji Na. 4 ya mwaka 1995 na kuanzisha upya Sheria ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa Zanzibar ya mwaka 2014, kwa madhumuni ya kuanzisha Serikali za Mitaa, uwezo wake, kazi na wajibu, muundo, mpangilio, fedha na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Waheshimiwa Wajumbe Mswada wa mwisho na wa nne ulikuwa ni Mswada wa Sheria ya kufuta Sheria za Tawala za Mikoa Na. 01 ya mwaka 1998, na kuanzisha upya Sheria ya Tawala za Mikoa ya Mwaka 2014 na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Kwa hivyo, Waheshimiwa Wajumbe kama inavyotakiwa chini ya Kanuni ya 91 (3) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi toleo la mwaka 2012, naomba kutoa taarifa kwamba Miswada hiyo sasa imekuwa sheria kamili, baada ya kusainiwa na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. *(Makofi)*

Nawashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe.

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Bismillahi rahmani Rahim.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe tuweke nidhamu vizuri.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, naomba kuwasilisha Mezani Nakala zote za Gazeti Rasmi la Serikali pamoja na vijalizo vyake kuanzia tarehe 1 Novemba. 2014.

Naomba kuwasilisha.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, naomba kuwasilisha Mezani Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Sheria ya Kupunguza na Kukabiliana na Maafa Zanzibar na Mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Naomba kuwasilisha.

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kuwasilisha Mezani Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Taasisi ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Uchumi Zanzibar na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Naomba kuwasilisha.

Mhe. Spika: Nafikiri Mheshimiwa Waziri samahani, mimi naomba kwamba Mswada huo usomwe kwa mara ya kwanza.

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Spika, naomba Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Taasisi ya Ulinzi ya Jeshi la Kujenga Uchumi ya Zanzibar na mambo mengine yanayohusiana na hayo, naomba usomwe kwa mara ya kwanza.

Mhe. Spika: Nimearifiwa tu kwamba hatua hiyo kumbe ipo mbele lakini nilisita kuita tena kuja kufanya hivyo itakuwa umefanya kazi hiyo kwa mpigo kwa ruhusa ya Spika, mpigo huo unaruhusika, tunaendelea.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kuwasilisha mezani Mswada wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Zanzibar, 2015

Naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 65

Utaratibu wa Polisi wa Faini za Papo kwa papo kwa Zanzibar.

Mhe. Ali Salum Haji **-** Aliuliza :-

Mhe. Spika, kabla ya kuuliza swali langu ningekuomba angalau sekunde 30 nitoe neno la shukurani kidogo tu.

Mhe. Spika, kwa niaba yangu na kwa niaba ya kamati yangu ya Ustawi wa Jamii ambayo inafanya kazi na Wizara tatu ikiwemo Ustawi wa Jamii na Uwezeshaji, Wizara ya Afya na Wizara ya Elimu. Na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kwahani napenda kutoa neno la pongezi na shukurani kwa Mheshimiwa Rais wa Zanzibar kwa kufuta kodi ya skuli za msingi Zanzibar. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kitendo hiki kimeonesha dhamira nzuri kwa Rais wetu kwa wananchi wake na kinakwenda na malengo ya kuendeleza kwa vitendo na dhamira, azma ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar. Tunamshukuru Mheshimiwa Rais na naomba tumpe mashirikiano katika ufanisi huu wa shughuli zake za kila siku.

Baada ya hayo Mhe. Spika, naomba sasa swali langu Na. 65 lijibiwe.

Kwa kuwa Jeshi la Polisi ni la Muungano, na kwa kuwa upande wa Tanzania Bara Jeshi la Polisi lina utaratibu wa sheria za faini ya papo kwa papo kwa vyombo vya moto vinavyovunja sheria za usalama barabarani.

Je, ni tatizo gani gani linalopelekea utaratibu huo kutotumika kwa upande wa Zanzibar.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais – Alijibu:-

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake nambari 65 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, Jeshi la Polisi ni Jeshi la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na limeundwa kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 chini ya Ibara ya 147 na kuanzishwa sheria chini ya Kifungu Nambari 3 cha Sheria ya Polisi na Polisi wasaidizi Cap. 322 R.E ya mwaka 2002.

Mhe. Spika, Miongoni mwa majukumu ya Jeshi la Polisi ni kusimamia na kutekeleza Sheria zilizotungwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar. Kwa upande wa Tanzania Bara, Sheria inayohusika na usalama barabarani ni Sheria nambari 168 ya mwaka 2002. Kwa kupitia Sheria hiyo, Jeshi la Polisi hutekeleza Sheria za faini ya papo kwa papo kwa vyombo vya moto vinavyovunja Sheria za usalama barabarani na kusaidia Serikali kukusanya fedha zinazotokana na madukhuli hayo.

Kwa hapa Zanzibar, Sheria Namba 7 ya mwaka 2003 (R.E 2006) ndiyo inayosimamia masuala ya usalama barabarani. Kwa mujibu wa Sheria hiyo, kifungu nambari 180 hadi 184 vimeelezea kuhusiana na utaratibu wa faini ya papo kwa papo kwa vyombo vya moto vinavyovunja Sheria za usalama barabarani.

Aidha, kifungu cha 184 cha Sheria hiyo kinamtaka Waziri anayehusika na barabara kutengeneza Kanuni ambazo zitakuwa zinakwenda sambamba na utekelezaji wa Sheria hizi.

Mhe. Spika, Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano tayari imeshatayarisha Kanuni za Sheria ya Usalama barabarani kwa upande wa Zanzibar na zipo Ofisi ya Mwanasheria Mkuu. Mara baada ya kukamilika kwa Kanuni hizo Jeshi la Polisi Zanzibar litaanza kuzitumia rasmi kwa kutoza faini za papo kwa papo kwa wale wote watakaofanya makosa ya usalama barabarani.

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Spika, namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri sana, lakini nataka nimueleze zaidi, kwa kuwa sheria hii Na. 07 ya mwaka 2003 ina karibu miaka miwili mpaka mitatu, tokea imeanzishwa yaani ya *On the Spot penalty*. Na kwa kuwa wenzetu Tanzania Bara wameweza kupata ufanisi wa namna mbili kupitia sheria hii ambayo imeanzishwa na Bunge, moja kuondosha mtiririko mkubwa wa kesi Mahakamani, lakini la pili kuongeza kipato kupitia faini za magari.

Nataka nimuulize Mhe. Waziri, kwa sababu amesema Sheria ipo kwa Mwanasheria lakini muda umekuwa ni mrefu. Je, anataka kutuahidi kwamba ni muda gani labda ambao unaweza kuchukua hata kumaliza *process* zake kutoka kwa Mwanasheria?

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Kwa kuwa namuelewa vizuri Mwanasheria Mkuu wetu mpya, nina hakika kwamba Kanuni hizi ambazo zimepelekwa na Waziri muhusika, zitakuwa tayari katika kipindi kifupi kijacho na zitaweza kutumika hapa nchini.

Mhe. Shadya Mohammed Suleiman: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa fursa hii kuweza kumuuliza Mheshimiwa Waziri swali moja la nyongeza.

Mhe. Waziri, kwa kuwa suala la ubora wa vifaa vya vyombo vya moto imekuwa tatizo mpaka kwa vipuri vyenyewe, Je, Serikali inaliangalia vipi suala hili?

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, naomba Mheshimiwa Shadya arudie kidogo swali lake pale mwanzo aliposema alisema nje ya Spika, kwa hivyo napata vigumu kumsikia naomba arudie kidogo.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, naomba kuweka sawa swali hili kumbe liko mbele yake sio katika suala hili.

Mhe. Spika: Mheshimiwa rudia swali lako kama bado una haja lijibiwe basi rudia swali lako.

Mhe. Shadya Mohammed Suleiman: Mhe. Spika, nimeridhika na majibu ya Mheshimiwa Waziri naomba aendelee *(Makofi)*

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, nakushukuru naomba nimuulize Mhe. Waziri swali la nyongeza lenye vifungu "a" na "b" kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amekiri kwamba Sheria Na. 7 ya usalama barabarani ni ya 2003 na hadi leo ni karibu miaka 12, haijatekelezwa kwa sababu ya kanuni za kuongoza sheria hiyo.

a)Haoni kwamba kuchelewa kwa Serikali kupitisha Kanuni ni mpango wa makusudi kwa Serikali ili ku-*support* rushwa?

b)Kwa sababu askari wetu wamekuwa wakipata tabu sana kwa sababu ya kukwama kwa kanuni hizi, ni lini sasa Mhe. Waziri atawafahamisha askari Polisi ili waache kuwasumbua wananchi kwa sababu kosa si wananchi kosa ni Serikali.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mheshimiwa sote ni mashahidi kwamba serikali yetu inafanya kila jitihada ya kupambana na rushwa nchini. Haina nia wala dhamira ya kuvutia kitendo chochote kile kinachoweza kuashiria mwanya wa rushwa.

Mhe. Spika, kwa hivyo nataka nimuhakikishie Mhe. Hija Hassan Hija kwamba unapotokezea ucheleweshaji wa kanuni si nia ya serikali ya kuvutia rushwa, bali ni utaratibu wa kawaida ambao wakati mwengine hujitokeza kwa sababu mbali mbali, lakini kwa kuwa sheria hii pia ilifanyiwa mapitio mwaka 2006, kwa hivyo sina shaka yoyote kwamba sasa baada ya Waziri husika kujiridhisha na kutengeneza Kanuni zinazofaa na kuzipeleka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu. Hivyo tutegemee kupata Kanuni bora kwa ajili ya utekelezaji mzuri wa sheria yetu na pia kupunguza usumbufu kwa kutenda vitendo vya uhalifu.

(b) Mhe. Spika, kuhusu swali (b) kwa vyovyote vile hairuhusiwi kuvunja sheria za barabarani. Unapovunja sheria za barabarani, japokuwa Kanuni hazipo, lakini bado sheria ipo inayoruhusu kuwakamata wale wote wanaovunja sheria hizo na kuwapeleka katika vyombo vya sheria ili sheria iweze kuchukua mkondo wake. Kwa hiyo askari wa Usalama Barabarani walikuwa wanafanya wajibu wao. wa kumkamata muhalifu yeyote yule anayevunja sheria za barabarani.

Mhe. Spika: Tunakushukuru Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na tunaendelea.

Nam. 14

Wanaume Kujitoga Masikio, Kusuka Nywele na Kujipodoa Zanzibar

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, ahsante sana, nami kabla ya yote naomba uniruhusu kwa dakika moja mpaka mbili na nusu nianze na utangulizi ufuatao.

Mhe. Spika, kwa heshima kabisa nichukue fursa hii nimshukuru Mwenyezi Mungu Allah (SW) baada ya kuachana kwa kipindi na hatimaye tunarudi tena humu tukiwa wazima wa afya, ni neema kubwa. Waheshimiwa Wajumbe, tumshukuru Mwenyezi Mungu kwa neema hiyo, huu si ujanja wetu, wala akili zetu, wala maarifa yetu.

Pili Mhe. Spika, nitakuwa sijakufanyia haki wewe uliyeniruhusu kusema maneno haya kukutakia afya njema na uendelee na kiti hicho.

Mhe. Spika, la tatu ambalo ni kubwa kuliko nililolikusudia ni kumshukuru Mhe. Rais wa Zanzibar kwa jitihada anazozichukua kwa wananchi wake wa Visiwa vya Unguja na Pemba, hasa katika sekta ya afya.

Mhe. Spika, hivi juzi Waheshimiwa Wajumbe wengine inaweza tukawa hatuna taarifa, si vibaya ikawa tunakumbushana. Kumefunguliwa ICU ya kisasa, naweza kuthubutu kusema hata Dar-es-Salaam haipo ICU hiyo. Baada ya kelele za Wawakilishi, ikiwemo na kelele za Mwakilishi wa jimbo la Muyuni. Niiombe Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Watoto wa Ustawi wa Jamii kile kitengo sio mas-hara, fedha nyingi zimetumika kwa kujengea hazipungui bilioni mbili.

Mhe. Spika, gharama ya kumlaza mgonjwa pale shilingi laki nane na hamsini elfu (850,000/-)kwa siku kama atatozwa. Lakini kutokana na umakini wa Dokta Ali Mohammed Shein wa kuwajali wananchi afya zao, kaweka bure. Kwa hiyo naiomba Kamati iweke pale angalau msafishaji wa masaa 24 ili pasije pakachafuka.

Mhe. Spika: Sawa tuendelee na swali sasa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: - Aliuliza:

Vitendo vinavyokwenda kinyume na maadili ya kijamii Zanzibar vimekuwa vikishamiri kwa kasi sana miongoni mwa vijana wetu na watu wa rika la kati. Viongozi mbali mbali wa kidini, wazee na walimu wamekuwa wakifanya jitihada ya kukemea vitendo hivyo bila kupata nguvu ya serikali inavyopasa. Kwa kuwa ni wajibu wa kikatiba wa serikali katika kulinda, kuimarisha na kuendeleza utamaduni wa Zanzibar, kwa mujibu wa kifungu cha 10 (f) cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984. Na kwa kuwa serikali imekuwa ikinyamaza kimya bila ya kuchukua hatua zinazopasa kudhibiti vitendo vinavyoharibu utamaduni wetu.

(a) Je, hatua gani kuanzia sasa zitachukuliwa na Serikali kutekeleza wajibu wake wa kikatiba kwa vitendo, na kupambana na uvunjifu huo wa mila, silka na desturi nzuri za nchi yetu.

(b) Kwa kuwa vitendo hivyo vinaipaka matope Zanzibar ambayo ni nchi iliyoshiriki kueneza ustaarabu wa dini na lugha ya Kiswahili Afrika, Serikali itachukua hatua gani za ziada ili sifa hizo zisipotee.

(c) Kwa kuzingatia ukubwa wa tatizo la mporomoko wa maadili ambao ni moja ya mambo yanayochangia kuongezeka kwa uhalifu na matendo ya uvunjifu wa amani, ni lini Serikali italeta mswada wa Sheria hapa Barazani utakaoweka adhabu kali kwa wanaume wanaofanya vitendo hivyo vya aibu.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Jaku Hashim Ayoub, kwa maelezo hayo na shukurani hizo kwa Mhe. Rais. Naomba sasa nimkaribishe Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 14 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, ni kweli vitendo vinavyokwenda kinyume na maadili ya kijamii vimekuwa vikishamiri kwa kasi miongoni mwa vijana wetu licha ya viongozi wa kidini, wazee na walimu kufanya jitihada kubwa ya kukemea. Lakini sio kweli kwamba Serikali haitilii mkazo juhudi za kukabiliana na hali ya uvunjifu wa mila, silka na desturi za nchi yetu. Baada ya maelezo hayo, sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, hatua zinazochukuliwa na serikali katika kupambana na uvunjifu wa mila, silka na desturi kama inavyotamkwa kwenye Katiba ni kushajihisha kutolewa elimu ya dini, na wazazi kulinda na kuhifadhi uendelezaji wa utamaduni wetu, pamoja na kuendeleza kusambaza ustaarabu wetu kwa njia ya sanaa, maonesho, semina na makongamano.

(b) Mhe. Spika, hatua nyengine zinazochukuliwa na serikali ni kuzipitia upya sheria zilizopo zinazohusiana na mambo ya mila, silka na desturi kwa lengo la kuzipa nguvu ili kupunguza kasi ya vitendo vinavyoipaka matope Zanzibar na vinavyomong'onyoa maadili ya nchi yetu ambavyo vinachangiwa sana na utandawazi.

(c) Mhe. Spika, serikali kwa ajili ya kukabiliana na uhalifu na vitendo vya uvunjifu wa amani sheria zipo na zinatoa adhabu kwa wakosaji. Tatizo lililopo si kutokuwepo kwa sheria bali ni usimamiaji wa sheria hizo na kuthibitika makosa mbele ya vyombo vya sheria ili kuweza kuchukuliwa hatua zinazofaa.

Mhe. Spika, kwa kulipatia ufumbuzi tatizo hili, sisi sote hapa ni viongozi, na wananchi kwa jumla tunatakiwa kushirikiana kupiga vita vitendo hivyo na kutilia nguvu usimamizi wa sheria zetu tunazozitunga.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu ya serikali naomba niulize swali moja la nyongeza lenye "a" na "b".

a) Mhe. Spika, kwa kuwa serikali siyo aghalabu kukiri, na hatimaye leo imekiri kuongezeka kwa vitendo vya mmong'onyoko wa maadili. Lini sheria hii italetwa humu ndani ya Baraza ili kuokoa nguvu kazi ya vijana na kulinda mila na desturi ya Mzanzibari.

b) Hatua za serikali kuruhusu baa mitaani na kuzipa baa vibali kwa kupiga muziki usiku kucha kama vile Bweni Cafe, Zebra Coconut. Hamuoni ndiyo chanzo kikubwa cha vijana kuporomoka. Mnatoa kauli gani kuhusu suala hili.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, kabla sijamjibu naomba nikiri kwamba Mhe. Jaku ni mmoja katika viongozi wanaokerwa sana na hali ya mmong'onyoko wa maadili katika nchi yetu.

Mhe. Spika, nakumbuka Mhe. Jaku, aliwahi kuja Ofisini kwangu na mabasi matatu ya wananchi wa jimbo lake; wa Paje, Muyuni na Jambiani, wakilalamikia kuhusu suala la matatizo la mmong'onyoko wa maadili yanayosababishwa na upigaji wa ngoma usiku kucha katika maeneo yao. Mazungumzo yetu na wananchi wake, kwa niaba ya serikali tumeyachukua na tumeyafanyia kazi.

Mhe. Spika, ndiyo maana katika kikao hichi, kwa ruhusa yako tutasoma kwa mara ya kwanza mabadiliko ya Sheria yanayohusiana na upigaji wa ngoma, mila, utamaduni na sanaa katika nchi yetu. Kwa hiyo lile ambalo unasema lini, ni kwamba kitakapoahirishwa kikao hichi na ratiba ambayo imetolewa na Katibu wa Baraza Mswada wa Sheria ya Mabadiliko ya Sheria ambayo iliyokuwa inaruhusu mambo hayo utasomwa mara ya mwanzo katika Baraza hili.

Mhe. Rufai Said Rufai: Mhe. Spika, na mimi sina budi kutoa shukurani zangu za dhati asubuhi hii kupata nafasi na mimi nikatoa swali langu dogo la nyongeza.

Mhe. Spika, kwa kuwa sheria za maadili zipo za tokea ukoloni na hadi baada ya ukoloni na sheria nyengine mbali mbali. Lakini hivi serikali kusimamia baadhi ya sheria na kutosimamia baadhi ya sheria. Je, serikali haioni kama inavunja sheria.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, Mheshimiwa Mwakilishi, tumeeleza kwa kina kwenye swali mama. Tumesema sisi sote humu ndani ni viongozi na sisi ndiyo tunaopitisha sheria. Sasa hivi sisi wenyewe binafsi tukiwa ni Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tuweze kusimamia sheria hizi tusione muhali. Kwa sababu sisi wenyewe tukiwa ni Wajumbe wa Baraza la Wawakili na ni viongozi, pale panapokiukwa maadili yetu ya Kizanzibari na kwenye jamii kutokana na mila potofu zilizokuwepo kwenye jamii.

Mhe. Spika, sisi wenyewe binafsi Waheshimiwa ndiyo tunaokwenda kusimama kidete kumuombea kwa sababu yule ni ndugu yako au ni mtoto wako ili aondokane na kadhia ile. Lakini nawaomba sana Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wanaofanyiwa matendo ambayo hayawezi kufanyika kwenye ubinaadamu, sisi wenyewe tusimame kidete. Kwa sababu sisi wenyewe ndio tunaopitisha sheria hizi tusimamie kwa kina, ili wale watu wanaoyaepuka maadili yetu ya Kizanzibari na wanaowadhalilisha watoto wetu tuweze kusimama kidete na tuweze kuelimisha jamii yetu kwa kina wasiwe woga waweze kutoa taarifa sahihi ili wahalifu wale waweze kuchukuliwa hatua za kisheria. Ahsante Mhe. Spika.

Nam. 51

Kuanzishwa Mtaala wa Pamoja kwa Madrasa Nchini

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, kabla ya swali langu Namb. 51 kujibiwa naomba nitoe kheri ya mwaka mpya, siyo tu kwa Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria lakini kwa Wazanzibari wote, Inshallah Mwenyezi Mungu atujaalie kila la kheri na kutupitisha mwaka huu salama usalimin. Aliuliza:-

Elimu ya Madrasa kwa vijana wetu ni muhimu sana, siyo tu kwa kuwajenga vijana hao katika “elimu ya kiroho” (Akhera) lakini vile vile kuwaweka katika maadili mema pamoja na kuendeleza mila na silka za Kiislamu hapa nchini. Kwa kuwa elimu ya madrasa utoaji wake ni mipango binafsi ya walimu na hakuna mitaala inayoeleza ufundishaji wake kwa nchi nzima.

Je, ni lini Afisi ya Mufti itaandaa utaratibu wa kutoa semina kwa walimu hawa kila baada ya kipindi fulani kwa Zanzibar nzima ili uwepo mtaala wa pamoja kwa madrasa zote.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 51 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, katika utekeleaji wa kazi zetu za kila siku tunalo lengo la kuzitambua Madrasa zote za Unguja na Pemba ili baadaye tupate wepesi katika kufanya mawasiliano na Madrasa hizo. Zoezi hili tumeshalianza na tumeshafikia takriban asilimia 70, hadi kufikia mwezi Disemba mwaka jana. Tarajio letu ni kulikamilisha katika kipindi hichi cha fedha, pale tu tutapopatiwa fedha za kutosha.

Mhe. Spika, pamoja na hayo Afisi ya Mufti wa Zanzibar kwa kushirikiana na baadhi ya washirika wa maendeleo na hasa *Global Network of Religions for Children (GNRC)* tumeshakubaliana kuendesha semina kwa Walimu wa Madrasa zote Kiwilaya kwa Madrasa za Unguja na Pemba. Katika semina hizo mada mbali mbali zitajadiliwa ikiwa ni pamoja na uwezekano wa kuwa na mtaala wa pamoja kwa Madrasa zote. Matayarisho ya shughuli hii yanaendelea vizuri na hivi karibuni tu Inshaallah tunatarajia kuendesha semina hizo.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri wa masuala ya Katiba na Sheria naomba niulize swali dogo la nyongeza kama ifuatavyo.

Kwanza nimpongeze kwa juhudi zake za kuweza kutambua hizi madrasa kwa asilimia 70 na kujaribu kutafuta huu muafaka kupata mtaala wa pamoja. Kwa kuwa madrasa zetu Mhe. Waziri zimetafutiana sana katika uwezo wa kujiendesha kwa kuwa nyengine zinapata ufadhili kwa mfano katika Taasisi za Kidini nyengine kama vile Istiqama, Zawiyatul Qadiriya, wanasaidia sana baadhi ya madrasa. Lakini kuna madrasa nyengine hazipati msaada hata katika taasisi hata moja, ni walimu wenyewe tu na wanakijiji wa Kijiji hicho, hawapati msaada wowote wa fedha kutoka Zawiyatul Qadiriya wala Istiqama,.

a) Je, ni utaratibu gani mtakaotumia serikali katika ku- *harmonize* uwezo wa hizi madrasa ili zisitofautiane katika mambo ya taaluma.

b) Mhe. Spika, kama nilivyosema madrasa nyengine hazipati chochote kutoka taasisi yoyote. Ni lini Serikali itaweka ruzuku maalum ili kuwasaidia walimu wa hizi madrasa ambazo ni masikini sana ambazo hazisaidiwi na Zawiyatul Qadiriya wala Istiqama, ziweze kupata fedha kidogo ili ziweze kujiendesha. Ni lini serikali itatoa ruzuku kwa madrasa hizi masikini sana zikiwemo zile za Vitongoji Umangani, Kibokoni, Wawi pale ambazo hazina msaada wowote.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika, ingelikuwa nataka nitumie Kanuni za Baraza suala hili ningekwambia kwamba tusilijibu lakini nitaomba nilijibu.

Kanuni ya Baraza inasema kwamba ikiwa swali limeshajibiwa kwa kipindi cha miezi sita huwezi tena kuliuliza. Mhe. Spika, swali hili nililijibu katika Kikao kilichopita na nikasema haya yafuatayo.

Mhe. Spika, madrasa zote ni za *private* sio za serikali na nakumbuka nilisema tuna madrasa kiasi 2,000. Nikasema kwamba serikali haiwezi kuzifanya madrasa hizi kwamba ni za serikali kwa sababu gharama zitakuwa kubwa sana kuzitia katika mfuko wa serikali.

Pia nilisema kwamba Ofisi yetu hata kama madrasa hizi ni za *private* lakini Ofisi ya Mufti inajaribu kupita na imeshapita, pale ambapo tunapata misaada tunatoa misaada kwa zile madrasa, tunatizama zile ambazo kidogo hali yao ni mbaya zaidi kuliko nyengine. Kwa maana hiyo hatuna ruzuku ya kuwapa isipokuwa tunawapa kile ambacho tunapata kimsaada au popote ambapo tunapata basi tunaweza tukawasaidia kwa misingi hiyo. Lakini hakuna ruzuku ya serikali ambayo tutawapa walimu wa madrasa ambao wanafika karibu 2,000. Nakushukuru.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru sana Mhe. Spika, kunipa fursa nimuulize Mhe. Waziri swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri anayosema Mhe. Waziri ya kuwa serikali itabeba mzigo mkubwa kwa kuhudumia madrasa ambazo zinafikia 2,000 katika Visiwa vyetu vya Unguja na Pemba.

Lakini kunatokea wafadhili kama anavyosema yeye mwenyewe wakasaidia hizi madrasa. Anasema wanasaidia zile madrasa ambazo zipo katika hali ya chini. Sasa Mheshimiwa kwa kuwa nchi yetu madrasa nyingi zipo katika hali ya

chini na hazina wafadhili na wakijitokeza hao wafadhili kusaidia ni utaratibu upi unaotumika ili na zile Madrasa nyengine ambazo ziko vijijini zifaidike na hao Wafadhili wanaokuja.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika, jibu langu ni kwamba wafadhili wanakuja Ofisini kwetu kama wana msaada wowote wanatupa, sisi Ofisini ndio tunaowa-*identify* ni madrasa zipi au vyuo vipi ambavyo vinapaswa kusaidiwa. Hayo yanafanywa na Ofisi zetu Unguja na Pemba. Nina hakika Micheweni tumeshasaidia madrasa hizo, nina hakika Nungwi tumeshasaidia, Makunduchi tumeshasaidia, Mkoani tumeshasaidia na maeneo mengine yote. Si wafadhili tunaowapeleka huko, ni Ofisi zetu za Mufti Unguja na Pemba ndio zina-*identify* sehemu ipi tutoe msaada na hivyo tunafanya.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Tokea kushika nafasi hiyo kubwa uliyokuwa nayo ni lini umekutana na walimu wa vyuo wa Unguja na Pemba kuwasikiliza kero zao, ili kuwasikiliza katika mahitaji yao ya kijamii.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika, walimu wa Unguja tumeshakutana nao, Ofisi ya Mufti kwa kushirikiana na Katibu Mtendaji wameshakutana katika sehemu tofauti. Walimu wa Pemba pia tumeshakutana nao katika misingi hiyo. Na kama nilivyosema mwanzo tunaendelea kukutana nao kila pale haja inapotokea na ndio maana nikasema katika jibu langu ni kwamba, hivi sasa tunazungumza na hawa *Global Network for Children* ili tuweze kufanya semina ya pamoja katika suala zima la kuelimishana, na kujaribu kuzungumza katika suala zima la madrasa ikiwemo masuala ya mitaala katika madrasa hizo. Na semina hizi nina hakika tukijaaliwa katika kipindi kifupi kinachofuata, kwa sababu hatua kubwa imeshafanyika, basi tutakutana nao tena kwa shughuli hizo.

Nam. 22

Ubovu wa Majengo ya Skuli Mpya za Sekondari Zilizopo kila Wilaya

Mhe. Panya Ali Abdalla - Aliuliza:

Ahsante sana Mhe. Spika, kabla ya kuuliza swali langu nilikuwa naomba ruhusa yako na mimi niweze kutoa shukurani zangu. Mhe. Spika, naomba nitoe shukurani kwa wajumbe wenzangu ambao walikuja kunifariji katika kipindi kizito nilichokuwa nauguza mtoto wangu. Napenda kuwashukuru kwa dhati na *inshaallah* Mwenyezi Mungu atawalipa heri na wale ambao hawakufika basi wasiwe na wasiwasi. Wale waliokuja walisema walikuja kwa niaba ya wenzao ambao nitakuwa siwaoni pale.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo naomba swali langu namba 22 lipate majibu.

Kwa kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imekuwa ikifanya jitihada mbali mbali ili kuwezesha wananchi wake kupata elimu bora kwa manufaa ya jamii nzima. Katika kuhakikisha jitihada zinafanikiwa, majengo ya skuli za kisasa yameendelea kujengwa katika maeneo mbali mbali ya Zanzibar, ili kuwawezesha wanafunzi kuwa na mazingira bora ya kujifunza. Na kwa kuwa, hivi karibuni umefanyika ujenzi wa skuli mpya za Sekondari katika kila Wilaya. Na kwa kuwa ujenzi wa baadhi ya skuli hizi haukuwa katika kiwango cha ubora, hali iliyopelekea skuli hizo nyingi kufanya nyufa za ubovu na athari nyengine mbali mbali zinazoonesha kuharibika kwa majengo hayo.

(a) Je, Serikali kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali inayo taarifa juu ya hali hiyo ya ubovu.

(b) Ikiwa Serikali inazo taarifa hizo, ni hatua gani zimeanza kuchukuliwa au zimepangwa kuchukuliwa ili kunusuru majengo hayo mapya, yasifikie hatua ya kuwa hayakaliki kabisa.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, naomba kumjibu Mhe. Panya Ali Abdalaa nafasi za wanawake swali lake Nam. 22 lenye (a) na (b).

Mhe. Spika, ni kweli kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imefanya juhudi kubwa katika kueneza huduma za elimu bora kwa wananchi wake wote. Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Dunia na Benki ya Kiarabu kwa Maendeleo ya Afrika (BADEA) imejenga skuli 21 za sekondari, imezifanyia ukarabati mkubwa skuli 6 za sekondari na imejenga *campus* mpya ya Chuo cha Ualimu cha Benjamin William Mkapa huko Mchanga Mdogo Pemba.

Ujenzi wa skuli hizo kumesaidia katika kuweka mazingira bora ya ufundishaji ambayo ni muhimu katika kuimarisha elimu.

Pia, ni kweli kuwa katika ujenzi huo, kumejitokeza kasoro kwa baadhi ya skuli. Kasoro hizo zinashughulikiwa kwa mujibu wa mikataba yetu ya ujenzi ambayo ina kipengele kinachomtaka Mkandarasi kufanya marekebisho pale panapogundulikana iwapo kwa kipindi cha mwaka mmoja kumetokea tatizo. Utaratibu huu ni wa kawaida katika mikataba ya ujenzi kwa kutarajia baadhi ya makosa yatajionesha wakati majengo yatakapoanza kutumika. Baada ya maelezo hayo, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake kama hivi ifuatavyo:-

(a) Wizara inazielewa kasoro zilizojitokeza katika ujenzi wa baadhi ya skuli mpya za sekondari.

(b) Wizara imeshachukua hatua kwa baadhi ya kasoro hizo kwa kuwataka Wakandarasi wafanye marekebisho kama hivi ifuatavyo:-

i) Skuli ya Faraja – Mkandarasi amefanya marekebisho ya ngazi inayotumiwa na wanafunzi wenye mahitaji maalumu.

ii) Skuli ya Maendeleo Ngwachani – Mkandarasi amefanya marekebisho ya nyufa zilizojitokeza katika baadhi ya kuta.

iii) Skuli ya Umoja ya Uzini – Mkandarasi amebadilisha *tiles* katika baadhi ya madarasa na jengo la utawala.

Kasoro moja kubwa iliyojitokeza ni kuvuja kwa baadhi ya mapaa ya baadhi ya skuli kunatokana na mabati kupitisha maji katika kiungo chake na ukuta. Kasoro hiyo imetokana na michoro waliyopewa Wakandarasi na Mshauri Mwelekezi. Dosari hii ni ya kiufundi na Wizara inaendelea kutafuta mshauri wa kitaalamu juu ya mbinu muhimu na bora za kuchukua kwa ajili ya suala hili.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante sana Mhe. Spika, niruhusu niulize swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri lakini ningependa nimuulize swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa lengo la Serikali lilikuwa nikupata elimu bora kwa wananchi wake pia elimu hiyo kupatikana katika majengo yaliyo bora. Je, Mhe. Waziri utakubaliana nami kwamba kuna umuhimu wa kufanya ziara za makusudi ya kuzitembelea skuli hizi za Sekondari mpya zilizojengwa, ili ukajionee wewe mwenyewe na kujiridhisha huo ukarabati unaofanywa na hizo athari ambazo zimejitokeza ili kuja kuepuka ule usemi wa kiswahili unaosema, *''bora kuziba ufa kuliko kujenga ukuta*''.

Mhe. Naibu Waziri uko tayari kufanya ziara hiyo na iwapo katika Mkoa wangu ukanishirikisha na mimi.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, nakubaliana na yeye na hizi kasoro ambazo nimesema kama tunazijua na tumezifanyia kazi ni kutokana na ziara zangu ambazo nilifanyia katika skuli hizo, tukagundua kama kuna kasoro hizi ambazo zimejitokeza na zikaanza kufanyiwa kazi. Lakini swali au ombi alilotaka kama nishirikiane na yeye katika Mkoa wake kuzifanyia tena ziara skuli hizi, niko tayari Mheshimiwa.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Ahsante Mhe. Spika, na mimi nichukuwe fursa hii kukutakia Mhe. Spika, wajumbe wenzangu na wazanzibari wote heri ya mwaka mpya, tuombe inshaallah mwaka huu umalizike kwa salama na amani na ulete mafanikio makubwa kwa wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Spika, naomba nimuulize Mhe. Naibu Waziri, swali la nyongeza lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo. Mhe. Spika, umeonekana umekuwa ni mtindo wa miradi mingi inayotekelezwa na Serikali hii, ujenzi wake kupata na hitilafu na kupelekea hasara kubwa kwa walipa kodi na wananchi wa nchi hii, kuhusiana na kadhia hii ya ujenzi wa Skuli za Sekondari zilizojaa matatizo. Nimuulize Mhe. Naibu Waziri:

(a) Kwamba haoni kuna haja ya kuwachukulia hatua watendaji wa Wizara yake na kwa Serikali kwa jumla ambao walihusika na usimamizi wa mradi huu wa ujenzi ambao umepelekea hasara kubwa.

(b) Serikali haioni kwamba kwa sababu suala hili limezungumzwa sana katika Baraza hili juu ya ubovu wa Skuli ambazo zimejengwa karibuni tu,kuna haja ya kufanya ukaguzi yakinifu wa miradi hii na ripoti yake kuletwa hapa Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, kama ambavyo nimezungumza kwenye jibu langu mama, nilisema kama kasoro hizi zimejitokeza katika baadhi ya skuli zetu, sio zote na ilitokana na mshauri mwelekezi ambaye alishirikiana na Msanifu wa Michoro na hili kosa si kosa la Wizara, kwa sababu katika ujenzi tatizo lolote linaweza likatokea. Hizi skuli Mhe. Spika, ni skuli 12 ambazo *plan* yake ni moja na katika skuli hizo 12 ni skuli tatu ambazo zimeonesha hilo tatizo. Ni skuli ya Kombeni, Chwaka Tumbe na skuli ya Madungu. Sasa ionekane kama si tatizo la Wizara, lakini ni tatizo la Mshauri ambaye katushauri katika michoro na inaweza ikatokea bahati mbaya, haiwezekani Mhe. Spika, kama skuli 12 zitokee skuli 3 tu matatizo.

Swali la pili aliliouliza kama Baraza la Wawakilishi lipewe fursa ya kupitia na kukagua juu ya hitilafu hizo ambazo zimetokea. Mimi Mheshimiwa sina tatizo na hilo kwa sababu moja ya jukumu la Baraza la Wawakilishi ni kusimamia Serikali.

UTARATIBU

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Naomba nimuweke sawa Mhe. Naibu Waziri, nilichouliza ni kwamba Serikali haioni kwamba kuna haja ya kufanya ukaguzi yakinifu sio Baraza ukaguzi kupitia Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Mahesabu ya Serikali juu ya miradi hii, ukaguzi yakinifu kwa maana ya *audit* ya *value for money*.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, ninashukuru kwa Mhe. Ismail kuniongoza kwenye suala. Mheshimiwa sina tatizo na hilo, kama kunaonekana kuna hitilafu yoyote ambayo imetokea katika utoaji wa tenda na mambo mengine yanayohusu ujenzi wa skuli hizo basi linaweza likafanyika hilo, sina tatizo nalo.

Mhe. Hamad Masoud Hamad: Mhe. Spika, na mimi vile vile kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kwamba mwaka huu wa 2015 Kikao chako kinafanyika Januari hii. Lakini pia niungane na wenzangu kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kututeua kuingia katika mwaka 2015 na inshaallah Mwenyezi Mungu aujaalie mwaka huu uwe mwaka wa mafanikio makubwa kwa watanzania.

Mhe. Spika, Mhe. Rais wa Zanzibar katika hotuba yake ya Sherehe za Mapinduzi miaka 51 alitamka kwamba skuli za *primary* elimu itakuwa bure. Kwanza mimi niipongeze kauli hiyo lakini niwatahadharishe walimu wa *primary* wamezoea miaka mingi kabla ya tamko hili, na kwamba tamko hili litaanza katika bajeti ya mwaka unaokuja, wasije wakageuka wakafidia elimu bure hiyo kwa kazi za mikono (*handworks). Handworks* ni kazi za kawaida lakini imegeuka ni kitega uchumi. Na kitega uchumi hiki kwa sisi ambao ni Wawakilishi tunapita maskuli inaonekana kwamba ni njia nyengine ya walimu kujiongezea mapato. Kwa hivyo, hii ni tahadhari tu na ninapongeza kwamba walimu wamepunguziwa kazi kubwa ya kukusanya hizi fedha ambazo zilikuwa ni malipo.

Sasa Mhe. Spika, niende kwenye swali, ninamuuliza Naibu Waziri wa Elimu, nini kadhia ya Skuli ya Mtule iliyoko baina ya kijiji cha Muungoni na Paje, pale kati kati iko skuli mpya Kitogani na Paje, na nini kadhia ya skuli inayojengwa Kizimkazi, njia panda pale ya Kizimkazi na Makunduchi, Kibuteni.

Lakini swali (b) ni kwamba je, Mhe. Naibu Waziri anaweza akatutajia Skuli hizi za Sekondari za Wilaya kila Wilaya imejengwa skuli ngapi au zitajengwa skuli ngapi. Ninakushukuru Mhe. Spika.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, alitaka kujua kadhia ya Skuli ya Paje Mtule na Skuli ya Kibuteni; kadhia ambayo iliipata Skuli ya Paje Mtule Mheshimiwa ni Mkandarasi ambaye hakuwa muaminifu. Baada ya Wizara kugundua kama Mkandarasi huyu hakuwa mwaminifu, ni mbabaishaji Wizara

ikachukua hatua ya kumzuilia kazi na ikatafuta mkandarasi mwengine mpya ambaye Mkandarasi huyo kafanya kazi vizuri na tayari skuli hiyo imemaliza ujenzi wake.

Skuli ya Kibuteni, hizi ni Skuli mbili; ni Skuli ya Kibuteni na Skuli ya Mkanyageni; skuli hizi Mheshimiwa bado hazijamalizika. Skuli ya Mkanyageni inaendelea na Skuli ya Kibuteni inaendelea na ujenzi na juzi tu katika Sherehe za Mapinduzi tulikuwepo Kibuteni na Waziri Mkuu kuweka jiwe la msingi la skuli hiyo.

Lakini pia Mhe. Hamad alitaka kujua skuli ambazo zimejengwa katika Wilaya zetu na ni skuli ngapi kwa kila Wilaya. Takriban kila Wilaya imepata skuli mbili na skuli wenyewe ni Kombeni, Chwaka Tumbe, Madungu, Matemwe, Uzini, Paje Mtule, Dole, Muwanda, Kiwani Mauani, Chasasa, Pandani na Wawi, ni hizo Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Kuna maelezo yoyote kuhusiana na swali lile la elimu bure kwamba walimu wale wasije wakaona kwamba sasa wafanye mpango mwengine kwa kazi za mikono kufidia naona alilitaja. Hebu kuna maelezo yoyote Mheshimiwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, katika kauli ambayo ameitoa Mhe. Rais juzi ya kufuta *fees* zinazotolewa na wazee kwa ajili ya Skuli za *Primary*, hili ni zuri Mhe. Hamad, amelizungumza na mimi nilitaka kuliweka sawa. Ni kwamba kwanza nitaanza katika mwaka mpya kwa sababu bajeti ya mwaka huu imemalizika, mwaka mpya wa fedha ndio ambapo litaanza kuchukua kazi tangazo hili. Na ni kweli alivyosema Mhe. Hamad, kuwa walimu wana njia mbadala za kupata fedha, lakini tutahakikisha tunafuatilia suala hilo na si hilo tu Mhe. Hamad, jana asubuhi saa moja na nusu nilikuwa Skuli ya Mpendae kutokana na kadhia ambayo walimu wanawarudisha watoto ambao hawakulipa. Nilikwenda kuzungumza na Mwalimu Mkuu na nikataka watoto wote warudishwe maskulini watalipa kwa mujibu wa uwezo wa wazee wao watakapopata.

Mhe. Spika, na hili nachukua fursa kutoa wito kwa walimu wetu wakuu katika maskuli yetu hakuna ruhusa ya kumrudisha mtoto nyumbani, watoto wote wana haki ya kusoma na ndio maana ikawa elimu ni bure tunachotakiwa ni kuchangia. Sasa mchango usiwe sababu ya kuwafanya watoto wa kimasikini ambao hawana uwezo wakakosa kusoma. Nakushukuru Mheshimiwa. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Na mimi nakushukuru sana.

Nam. 88

Utaratibu wa Kuchunguza Bidhaa Feki

Mhe. Ali Salum Haji - Aliuliza:-

Kutokana na ukuaji wa biashara kumejitokeza baadhi ya wafanyabiashara kuingiza bidhaa ya vilainisho feki; mfano girisi na *oil* za vyombo vya moto, wenzetu Tanzania Bara kupitia Ofisi ya Mkemia Mkuu wameanzisha ukaguzi wa bidhaa hizo kupitia *'ICP machine'*. Je, Zanzibar ina utaratibu gani wa kuchunguza bidhaa kama hizo?

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko – Alijibu:-

Mhe. Spika, ahsante kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 88 kutoka kwa Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, ni kweli kwamba vilainisho vinavyoingia nchini bado havijapata vipimo stahiki ambavyo vipimwe na kuhakikishiwa watumizi wake ubora wake. Kwa sasa tunapima vilainisho pale ambapo mteja anapohisi kwamba kadhulumiwa au kitu alichouziwa sio barabara, tunachukua *samples* hizo na kuzipeleka nchi za jirani hasa Tanzania Bara kwa kupima kutokana na sheria ya kumlinda mtumiaji. Lakini hasa kazi hii inabidi ifanywe na *Zanzibar Bureau of Standards,* lakini kwa bahati mbaya mpaka sasa hivi tumo katika kukiimarisha kitengo chetu cha *ZBS* na bado hatujakuwa na maabara za kuweza kupima vitu hivyo.

Kwa hivyo, *ICP machine* hatuna kwa sasa hivi, kwa hivyo, ni kweli kwamba mpaka sasa hivi hatupimi kitaalamu vifaa hivyo ila tunaangalia *expiry date* na *date of manufactory* na mambo mengine.

Hivyo basi, naomba niwahakikishie kwamba wizara yetu inafanya kila aina ya juhudi kuona kwamba *Zanzibar Bureau of Standards* inafanikisha kupata maabara moja hadi nyingine na katika maabara za mwanzo zitakazoimarishwa ni maabara ya kupima vilainisho vya magari. Ahsante.

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mhe. Waziri, kwanza nimshukuru sana na nimpongeze kwa kujibu ukweli wa hali halisi ilivyo hasa. Lakini nilitaka nimuulize swali jingine dogo tu kwamba kwa kuwa wizara sasa hivi inajitayarisha kupata hiyo *machine* ya *ICP* ili kuweza kupimia vilainisho.

Mhe. Spika, lakini nataka nimueleze Mhe. Waziri, kwa kuwa ni bidhaa feki, sio vilainishio, pia kulijitokeza wimbi la bidhaa la vipuri vya magari kwa mfano *machine* na *piston* yaani vipuri vya aina mbali mbali ambavyo vinakuwa vinakuja havina viwango, yaani mtu anapokitia hakichukuwi muda kinapasuka.

Mhe. Spika, na kwa kuwa wenzetu Tanzania Bara wameanzisha utamaduni wa kupita madukani kutafuta bidhaa feki, kwa mfano juzi walibaini simu ambazo hazina kiwango, ambazo zinahatarisha afya ya mwanadamu, lakini pia zinagharimu wananchi kuwapa gharama ambazo hazina msingi.

Je, na hili nalo Mhe. Waziri analiangalia vipi katika upande wa bidhaa feki za vipuri vinavyoingia katika nchi yetu.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, ni kweli bidhaa feki ni nyingi zikiwemo simu, vipuri vya magari na mengineyo. Lakini *ZBS* kwanza ili iweze kuimarisha maabara zote tisa za kufanya kazi hiyo, zinahitajika fedha si chini ya bilioni 12, si kweli kama tutaweza kufanya kila uwezo wa kuweza kuimarisha maabara zote 12 kwa muda huu, lakini tukaanza moja hadi nyingine. Lakini basi, naomba kuwashauri wananchi wote wanapohisi wameuziwa bidhaa feki, basi sheria ya kumlinda mtumiaji ipo watuletee bidhaa hiyo na wako wananchi bidhaa hizo wanatuletea na wakituletea bidhaa hizo sisi tunachukua hatua za kisheria kwa mujibu wa sheria ya kumlinda mtumiaji na sheria ipo kwa anayeuza kitu feki inatiwa adabu inayostahiki.

Naomba tena wananchi wote pamoja na wawakilishi kutoka Baraza hili kwamba *Zanzibar Bureau of Standards* ndio imeanza kazi karibuni mchakato huu wa muda mrefu si muda mfupi. Kwa hivyo, tuwe wavumilivu, lakini naamini kwamba hatua kwa hatua tutafikia malengo, mwananchi yeyote anahisi kauziwa kitu feki asinunue, akinunua akiona kadhulumiwa aje wizarani, zipo njia sahihi kabisa za kumshtaki yeyote yule ambaye kwamba ameuza kitu feki. Ahsante.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Spika, ahsante sana na mimi asubuhi ya leo hii kuweza kunipa nafasi ya kuweza kumuuliza Mhe. Waziri maswali mawili la nyongeza.

Mheshimiwa nashukuru sana kwa majibu yako mazuri na yako wazi. Mheshimiwa katika swali mama ulisema ni kweli na umekiri kuwa hamutumii vifaa vya teknolojia ambavyo vinaweza vikachunguza na vikatoa jibu sahihi, isipokuwa mnatumia katika suala la *expiry date.* Je, Mhe. Waziri huoni kusema hivyo unaipunguza nguvu wizara yako.

Mheshimiwa, lakini pili nilishtuka sana ulivyosema kuwa mnachukua vitu hivi na kuvipeleka Bara kwa kufanya utafiti wakati sisi tuna kitengo chetu cha *ZBS*. Sasa je, Mheshimiwa huoni kama iko haja sasa kitengo hiki ukatafuta zana zilizokuwa zinakwenda na wakati kuliko kwenda sehemu nyingine.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mheshimiwa Mshimba ahsante, suala la kwanza naona nimeeleweka vizuri sana kwamba bado *Zanzibar Bureau of Standards* haina maabara ya kuweza kupima hivyo vilainisho na vitu vyingine hivyo. Hata hao *TBS* wametumia muda wa miaka 15, ndio wamefikia hatua ambayo wamefikia sasa hivi, tena basi maabara zao nyingi hao *TBS* wamesaidiwa na wafadhili mbali mbali. Na mpaka sasa hivi vile vile kuna maabara nyingine hapo *TBS* hawana uwezo wa kupima vinavyopelekwa Nairobi na vyingine vinapelekwa South Africa mpaka hivi sasa.

Kwa hivyo, si jambo rahisi kwamba *Zanzibar Bureau of Standards* itaweza na vitu vyote hivyo kwa wakati mmoja. Lakini tunayofanya sasa hivi jitihada ya kuona kwamba *Zanzibar Bureau of Standard* iweze kusimama kwa miguu yake miwili, iweze kupima bidhaa hizo na tutaanzia na bidhaa za vyakula vya aina yote, tutakwenda katika bidhaa za vitu vya hatari kama vile *condoms* na bidhaa nyingine, pia tutakwenda katika bidhaa za magari. Kwa hivyo,

tutakwenda hatua kwa hatua, si rahisi na nitakuwa nakudanganya na sitakutendea haki kukwambia kama tutaweza kufanya hiyo kwa sasa hivi.

Njia ambayo wenzetu wengine wanatumia wote duniani ni kuajiri mashirika makubwa duniani ambayo yanafanya *test* huko huko kabla mzigo haujaingia nchini, mzigo ukinunuliwa tu basi unafanyiwa utafiti kule kule na inapatikana *clearing certificate* ambayo inaitwa *PVOC***.** Sisi Zanzibar bado utaratibu huo hatujauanza, serikali bado imo katika utafiti ikiwezekana basi tutaweza kutumia maabara za kimataifa ambazo kwamba mizigo inachekiwa kabla ya kuitoa ndani ya kontena kwanza ithibitishwe ubora wake.

Naomba mutuamini kama wizara hii hatufanyi mchezo kwa hilo tunalisimamia kwa visigino kuona kwamba tunaweza kwa muda mfupi kufika malengo hayo, wala hatukusudii kuidhalilisha Wizara ya Biashara au kuidhalilisha Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar, lakini uwezo wetu wa kifedha haukidhi haja ya kufanya mambo yote hayo. Lakini kwa mujibu wa uwezo tulionao na kwa mshahara tunaopata naamini katika kipindi kifupi *Zanzibar Bureau of Standard* itaweza kufanya mambo mengi sana ambayo nyote mtafurahia. Ahsante.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Spika, ahsante sana pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri naomba niulize swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa uwezo wa wateja kuweza kujua ufeki wa baadhi ya vifaa ni mdogo na kwa kuwa vilainisho vingi si rahisi kuvijua kwa kuviangalia sisi watu wa kawaida. Na kwa kuwa kwa sasa kuna ongezeko kubwa la hewa ukaa na hizi *fake oils* hizi zina *emission* kubwa ya *common oxide* jambo linasababisha hewa ukaa nyingi katika mazingira jambo ambalo linaweza likaathiri watumiaji pamoja na wananchi kwa ujumla.

Je, ni lini serikali inaweza ikanunua hii *ICP machine* na ni juhudi gani za haraka ambazo zitafanya serikali ili iweze kununua hii *ICP machine* kwa kunusuru mazingira yetu kuharibiwa na hewa ukaa kwa kiasi kikubwa, hilo ni moja.

Pili, je, serikali inaweza ikatueleza kwamba imeshindwa kununua *ICP* kama vile ilivyoshindwa kununua *machine* ya vinasaba, jambo ambalo ni tatizo katika nchi hii hadi leo hii kwenye Mahakama zetu.

Mhe. Spika: Mheshimiwa rudia swali lako.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Nasema kwamba serikali hadi leo hii imeshindwa kupata ile *machine* ya kupimia *oils,* sababu iliyoshindwa serikali kupata hii *machine* ni ughali wa *machine* hii kama ilivyoshindwa kununua *DNA machines*.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, namshukuru sana Mhe. Mwakilishi kwa maswali yake ni kwamba siwezi kujibu suala la *machine* ya *DNA*, lakini naweza kujibu *machine* ya *ICP*.

ICP ni *machine* moja tu kati ya *machine* zinazohitajika na *ZBS, ZBS* inatakiwa iwe na maabara zisizopungua tisa na maabara ya kwanza basi ya *ZBS* ni maabara ya kuthibitisha *equipments* zote ambazo zinatumiwa na maabara zote nchini hiyo ya kwanza na nyingine tena ije ya vyakula, nguo, ngozi na vitu vya vipodozi, kwa hivyo, kwa kweli mradi huu ni mkubwa sana.

ICP machine ni moja tu katika *machine* hizo, lakini *machine* ni nyingi. Sasa sisi tumesema kwamba tunakwenda hatua kwa hatua, tunataka *machine* nyingi sana sio *ICP* tu hata huko hospitali umesema ni *DNA,* lakini ziko *machines* nyingi sana huko hospitali vile vile, lakini mimi sitaki kuzungumza habari ya *DNA*, nasema kwamba sisi Wizara ya Biashara na Masoko kupitia Taasisi yake ya *Zanzibar Bureau of Standard* tutahakikisha kwa kipindi kifupi kijacho tunanunua *machine* ya *ICP* ili kuondoa mzozo huu wa kupata hewa chafu katika nchi yetu. Naamini kwamba *concern* ya wawakilishi juu ya suala hili ni kubwa. Kwa hivyo, *concern* ya wawakilishi ndio *concern* ya wananchi na serikali hii ni serikali ya wananchi, kwa ajili ya wananchi na inawatumikia wananchi. Kwa hivyo, tunawakikishia kwamba tutanunua *machine* hii ili tuoneshe kwamba tunawatumikia wananchi. Ahsante.

HOJA ZA SERIKALI

Mswada wa Sheria ya Kukabiliana na Maafa Zanzibar, 2015

(Kusomwa kwa mara ya Kwanza)

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, naomba kuwasilisha Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Sheria ya Kupunguza na Kukabiliana na Maafa Zanzibar na mambo mengine yanayohusiana na hayo ili kusoma kwa mara ya kwanza.

Mhe. Spika: Kwa upande wa Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, kazi hiyo tuliifanya kwa mpigo kwa ruhusa ya Spika, tuendelee Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais (Kny: Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ): Mhe. Spika, naomba kuwasilisha Mswada wa Sheria wa Kuanzisha Taasisi ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Uchumi Zanzibar na Mambo yanayohusiana na hayo ili kusomwa kwa mara ya kwanza.

Mhe. Spika: Haya ni mara ya pili mnawasilishwa kusoma kwa mara ya kwanza tumkaribishe Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kuwasilisha Mswada wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Zanzibar ya Mwaka 2015 ili uweze kusomwa kwa mara ya kwanza. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Spika: Ahsante sana Waheshimiwa muongozo wa Spika, Mhe. Ismail Jussa Ladhu.

MUONGOZO

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, Baraza lako katika kuhakikisha ufanisi wa utendaji wake la kuwapa nafasi vizuri wawakilishi kuweza kuwawakilisha ipasavyo wananchi ulianzishwa utaratibu mzuri sana wa kusomwa Miswada ya Sheria mara tatu, moja wapo ikiwa ni kutaka maoni ya wananchi.

Mhe. Spika, hoja yangu kwa muda huu ninayotaka muongozo wako ni kwamba, kwa sababu ya kutokuwa mwenyeji sana wa Kanuni zako za Baraza naomba unisaidie kwamba ni sahihi kwa waziri kuwasilisha mezani kwanza na baadae kuwasilisha kwa kusomwa mara ya mwanzo Mswada ambao Wawakilishi mpaka dakika hii hawajapewa?

Mhe. Spika, nauliza suala hili kwa sababu Mswada wa mwisho ambao uliwasilishwa mezani kwanza asubuhi na pili tunaambiwa umewasilishwa kwa mara ya kwanza, yaani kusomwa kwa mara ya kwanza, kwa maana ya Mswada wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Zanzibar, 2015 mpaka dakika hii Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi hawana nakala yake. Nataka kupata muongozo wako Mhe. Spika, jambo hili ni sahihi? Ahsante.

Mhe. Spika: Nakushukuru sana Mhe. Ismail Jussa Ladhu, Miswada inayowasilishwa kwa hati ya dharura kimsingi inatakiwa ipatikane kwa Waheshimiwa Wajumbe ili Waheshimiwa na hasa zaidi wale wanaohusiana na Kamati zinazohusiana na miswada hiyo wapate kwenda kuishughulikia katika Kamati. Kwa sababu licha ya kwamba miswada hiyo imekuja kwa hati ya dharura, lakini Kamati zinaweza zikenda zikashughulikia miswada hiyo kwa mujibu wa Kanuni ya 83(3) na 83(4).

Sasa nimearifiwa kwamba miswada hiyo ipo tayari, hiyo ya mazingira mingine iligawiwa jana, lakini hiyo ya dharura iko tayari imefika hivi asubuhi mara tukitoka humu ndani itagawiwa kwenu miswada hiyo kwenu Waheshimiwa Wajumbe. Kwa sababu hiyo, ndio ikawa tumekubaliana, tulitaka tuuondoe Mswada huo wa Mazingira ili isisomwe kwa mara ya kwanza, lakini mara baada ya kuarifiwa kwamba iko tayari nikaruhusu usomwe kwa mara ya kwanza ili Wajumbe wa Kamati inayohusika nao watakabidhiwa pamoja na Wajumbe wengine ili miswada hiyo ikashughulikiwe na Kamati.

Kwa hiyo, muongozo huo kwamba na huo pia Mswada wa Mazingira usomwe kwa mara ya kwanza nilitoa mimi iingie katika *order paper* hii baada ya kuridhika kwamba miswada hiyo iko tayari na itagawiwa hivi punde kwa Waheshimiwa Wajumbe.

Basi baada ya hayo nataka nitoe maelezo yafuatayo:-

Waheshimiwa Wajumbe, miswada mitatu ambayo imeorodheshwa hapo kwa mtiririko kama unavyoonekana ni miswada ambayo imekuja kwa mujibu wa hati ya dharura ya mkono wa Rais, ili iingie katika shughuli za Baraza katika mkutano huu. Kwa kawaida miswada hiyo inayokuja kwa hati ya dharura huwa haina nafasi ile siku 21 kutangazwa katika gazeti rasmi kwa sababu imekuja kwa dharura. Kamati bado pamoja na dharura hiyo, zinategemewa zifanye kazi ya kuipitia na waridhike kwamba iko tayati sasa kuweza kuwasilishwa kusomwa kwa mara ya pili ili mjadala uendelee, lakini hatua hiyo ya Kamati bado haijafanyika.

Kwa hiyo, kwa mujibu wa Kanuni ya 83(3) na 83(4) miswada hiyo haitaweza kusomwa kwa mara ya pili leo kwa kuwa Kamati bado hazikupata nafasi ya kupitia na hatimaye kumuarifu Spika kwamba miswada hiyo sasa ipo tayari kwa ajili ya kusomwa kwa mara ya pili na mjadala kuendelea na hatimaye kufikishwa kwa kusomwa kwa mara ya tatu.

Hivyo, kufuatana na sababu hiyo na kwa umuhimu wa Kamati kwamba zikapitie miswada hiyo nachukua nafasi hii kusitisha shughuli za Baraza kuanzia sasa ili mara tukiondoka humu ndani tuweze Kamati zinazohusika kwenda kuipitia miswada hiyo kwa mriritiko huo na tunategemea kwamba miswada hiyo ije iwasilishwe kwa kusomwa mara ya pili, Mwenyezi Mungu akitujaalia kuanzia kesho kwa mtiririko huo huo kama ilivyoonyeshwa kwenye *order paper* ya leo. Bila shaka itafuata na kazi za Kamati kumalizika kwa ufanisi wa kiasi gani.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wajumbe, baada ya maelezo hayo tukubali kusitisha shughuli zetu saa hizi hadi kesho tarehe 22/01/2015 saa tatu barabara za asubuhi ili kuzipa nafasi Kamati zinazohusika zikashughulikie miswada hiyo kuanzia sasa. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wajumbe, kikao hiki sasa kinaakhirishwa hadi kesho tarehe 22/01/2015 saa tatu za asubuhi.

(Saa 4:26 asubuhi Kikao kiliakhirishwa hadi tarehe 22/01/2015 saa 3:00 asubuhi)